

"Akina mama ndio watoa huduma wa pekee au wa msingi katika nyumba nne kati ya kumi….milioni 8.6 (63%) ni akina mama wasio na waume. - *Kituo cha Utafiti cha Pew*

"Wahasiriwa wa ukatili wakijinsia mara nyingi wanakabiliwa na ubaguzi katika makazi, kama vile kufukuzwa au kukataliwa kwa makazi kulingana na dhuluma waliopatwa nayo au unyanyasaji wa kingono mikononi mwa wamiliki na wasimamizi wa nyumba."

*-Shirika la Haki za Umma la Marekani*

"Kupata makazi yaliyo salama na ya bei nafuu ni sehemu muhimu ya usalama wa kiuchumi kwa watu wote,lakini wanawake wa LGBT mara nyingi hulipa bei isiyofaa katika soko la makazi kwa sababu ya mwelekeo wao wa kimapenzi au kitambulisho cha kijinsia."

*-Kituo cha Maendeleo ya Marekani na Mradi wa Maendeleo ya Harakati*

"Sisi sote tunafaidika kijamii, kisiasa na kiuchumi kutoka kwa usawa wa kijinsia katika maisha yetu ya kila siku. Wakati wanawake wanawezeshwa, wanadamu wote wanafaidika. Usawa wa kijinsia hukomboa sio wanawake tu bali pia wanaume, kutoka kwa majukumu yaliyowekwa ya kijamii na ubaguzi wa kijinsia."

*-HeForShe*

*Harakati ya Mshikamano wa Wanawake wa Usawa wa Jinsia ya Umoja wa Mataifa*

EQUAL HOUSING OPPORTUNITY

Ikiwa unafikiria kwamba umebaguliwa katika shughuli ya kupata makazi, wasiliana na:

Ushirikiano wa Usawa wa Makazi wa Northwest
35 W. Main Ave, Suite 250
Spokane, WA 99201

Nambari ya simu. 509-325-2665
1-800-200-FAIR (3247)
Faksi: 1-866-376-6308
www.nwfairhouse.org

Tunaweza kukushauri juu ya machaguo yako na kukutetea. Huduma zetu ni za bure.

**HUD-Makazi na Maendeleo ya Mjini**
**Alaska, Idaho, Oregon na Washington**
1-(800)-877-0246 www.hud.gov

**Tume ya Haki za Kibinadamu ya Jimbo la WA**
1-800-233-3247 www.hum.wa.gov

**Simu ya Kitaifa ya Dhuluma ya Nyumbani**
1-800-799-7233 and 1-800-787-3224 (TYY)
www.thehotline.org

**Mradi wa Haki za Wanawake wa ACLU**
(212) 549-2644
www.aclu.org/womensrights

Kazi ambayo ilitoa msingi wa chapisho hili iliungwa mkono kwa sehemu na ufadhili chini ya ruzuku kutoka Idara ya Makazi na Maendeleo ya Mjini ya Marekani. NWFHA inawajibika kikamilifu kwa taarifa na tafsiri zilizomo katika chapisho hili. 3/16

# Wanawake na Usawa wa Makazi



## Ulinzi katika kukodisha au kununua nyumba

"Nyumba na makao ambayo ni salama, ya bei nafuu na inayofaa ni kipimo cha ubora wa maisha ambao kila mwanadamu anatamani."

*Wanawake na Makazi: Kuelekea Miji Jumuishi Programu ya Umoja wa Mataifa ya Makazi ya Binadamu*

**USHIRIKIANO WA USAWA WA MAKAZI WA NORTHWEST**

(509) 325-2665
1 (800) 200-FAIR (3247)
www.nwfairhouse.org

# Kukodisha



Tafuta nyumba unayoweza kumudu na katika eneo unalopenda. Tembelea eneo hilo kwa nyakati tofauti kuona kama kitongoji kinakidhi mahitaji yako.

Pata nyaraka na mikataba ya makazi katika maandishi. Weka nakala za rekodi zako kila wakati (kwa mfano: matangazo, mikataba ya kukodisha, viambata, risiti za kodi, notisi, maombi ya kukarabati, na malalamiko).

### Mifano ya ukiukwaji wa usawa wa makazi:

- Ni kinyume cha sheria kwa mtoaji wa nyumba kukukataza makazi, au kusitisha upangaji kwa sababu wewe ni **mjamzito** au umepata ujauzito.

- **Unyanyasaji wa kingono** na wamiliki wa nyumba, mameneja, au wafanyakazi wa matengenezo ni haramu. Kuitisha hisani za kingono ili kupata makazi, kuweka makazi au kama malipo ya ukarabati, vifaa, au kodi ni kinyume cha sheria. Meneja pia ana wajibu wa kutoa makazi bila unyanyasaji wa kingono kutoka kwa wapangaji wengine na lazima atoe onyo kwa wanaokiuka ikiwa ni pamoja na kusitisha upangaji ikiwa itaendelea.

- Kukataa kumkodishia mwanamke au kusitisha upangaji wake kwa sababu yeye ni mhasiriwa wa **dhuluma ya nyumbani** ni kinyume cha sheria.



# Ulinzi wa Serikali: Jinsia

Sheria ya serikali ya Usawa wa Makazi inalinda watu dhidi ya ubaguzi wa makazi kwa sababu ya jinsia au kitambulisho cha kijinsia.



### Ulinzi wa Ziada wa Serikali

Sheria ya serikali **"Usawa wa Ufikiaji"** inawalinda watu wa LGBT (wasagaji, shoga, wanaopenda jinsia zote mbili, waliobadilisha jinsia) ambao wanapatwa na ubaguzi wa makazi katika mipango ya serikali inayohusiana na makazi ya bei nafuu na ukopeshaji.

**Urekebishaji Upya wa Sheria ya Ukatili Dhidi ya Wanawake** (VAWA) inapanua ulinzi wa makazi kwa wahasiriwa wa dhuluma za nyumbani, dhuluma za uchumba, na ushambulizi wa kingono.

### Ulinzi wa Jimbo la Washington

**Sheria ya Jimbo la Washington Dhidi ya Ubaguzi** (WLAD) inakataza ubaguzi kwa msingi wa jinsia, mwelekeo wa kimapenzi, na kitambulisho cha kijinsia. Hii ni pamoja na marufuku ya ubaguzi dhidi ya wanawake wajawazito.

# Umiliki wa Nyumba



Kabla hujaanza kutazama nyumba, fanya utafiti kwenye **mabenki na wakopeshaji.** Jifahamishe kuhusu mikopo **inayopatikana** na upate baruaya kuhitimu kutoka kwa mkopeshaji wako. Sio lazima ununue nyumba kwa kiasi kamili, lakini jua machaguo yako.

Katika jimbo la WA, ikiwa wewe ni mwanamke ambaye ni mseja, una mwenzi, umeolewa, umetalikiwa, ni mjane, unapenda watu wa jinsia tofauti, ni wa LGBT, ni mjamzito, una watoto au sio mama, wakopeshaji wanahitajika kukuhudumia kwa njia sawa na waombaji wengine wakati wa kushughulikia **ombi lako la mkopo**.

Kuwa na mahojiano na **maajenti wa uuzaji wa nyumba.** Uliza marafiki na familia wakujulishe maajenti ambao wametumia na wamependa na upate mtu anayekufaa.

Chagua **nyumba** ambayo unapenda, inayokidhi mahitaji yako, na ambayo unaweza kumudu. Ni kinyume cha sheria kwa mtu anayekusaidia kupata nyumba kukuelekeza katika mahali ambapo "unaweza kujisikia huru zaidi" au "pana watu wengi kama wewe."

### Mifano ya ukiukwaji wa makazi:

- Ikiwa wewe ni mjamzito na unatafuta mkopo wa nyumba, benki au mkopeshaji hapaswi kukukataza mkopo kwa sababu utakuwa ukienda **likizo ya uzazi** au kuchelewesha kukupa mkopo mpaka urudi kazini.

- Kupewa nukuu ya juu **ya bima** kunapaswa kuwa kulingana na sifa za nyumba wala sio jinsia yako au kitambulisho chako cha kijinsia. Zunguka ukitafuta.